
# JARIDA LA ATD DUNIA YA NNE TANZANIA

Jarida la kwanza la mwaka 2021

## Tahariri



Wapendwa marafiki wa ATD Dunia ya nne, ni matumaini yetu kuwa mpo salama huku mukiendelea na shughuli za kila siku za kijamii na kiuchumi ili kuhakikisha kuwa tunatokomeza umaskini mwezigoni mwetu.

Pia tunayofuraha kuwakaribisha kusoma jarida letu la kwanza kwa mwaka huu 2021,

Katika jarida letu tutaeleza namna ambavyo janga la korona limeathiri jamii maskini na namna ambavyo tulishirikiana na kupambana kwa pamoja, maadhimisho ya siku ya kimataifa ya kutokomeza umaskini uliokithiri katika jamii ambayo yaliazimishwa tarehe 17, Oktoba, 2020, ambapo kauli mbiu ya siku hiyo ilikuwa ni **"kuchukua hatua kwa pamoja ili kufikia haki za kijamii na mazingira kwa wote".**

Pia tutaeleza juu ya ukaribisho wa wageni ambao ni wafanya kazi wa kujitolea wa ATD Dunia ya nne na pia tulivyowaaga ndugu zetu Salma na Salehe ambao pia ni wafanyakazi wa kujitolea wa ATD Dunia ya nne ambao wamehamia mkoani Njombe kwa ajili ya majukumu ya harakati za kupambana na kutokomeza umaskini.

Mwisho kabisa ni ukurasa ambao utakuwa umesheheni picha za matukio mbalimbali.

Hayo ni yale ambayo kwa pamoja tuliweza kuyashuhudia na kuyatekeleza kwa mwaka 2020.

Tuungane kwa pamoja kuendeleza mapambano dhidi ya umaskini uliokithiri katika jamii zetu.

**Hamisi I. Matibu, mwanaharakati wa ATD dunia ya nne Tanzania**



Iwapo serikali itaamua kuongeza muda wa masharti ya korona, athari zake kwa watoto kutoka familia maskini zitakuwa mbaya kwa sababu watasahau yote waliyojifunza shuleni…! Alisema Halima kutoka Tegeta mwanzoni mwa

**Janga** la **korona** limebadili taratibu za maisha duniani kote. Utendaji na taratibu za taasisi na serikali mbalimbali umebadilika kulingana na ukubwa wa janga lenyewe katika maeneo tofauti. Katika maeneo mengi duniani watu wanaendelea kuathirika.

Serikali ya Tanzania ilichukua tahadhali kadhaa kukabiliana na janga la korona mara lilipoingia nchini mwanzoni mwa mwezi Machi 2020. Wananchi walihamasishwa kufuata njia sahihi kiafya kuepuka matokeo hasi yanayoweza kutokana na janga hili. Matamshi hamasishi sahihi pamoja na juhudi za vitendo, yote haya yalisaidia kuwajenga wananchi kisaikolojia hivyo kuwaondoa katika hofu na kuchukulia korona sawa na magonjwa mengine yaliyopo nchini.

Hadi mwezi June 2020, wananchi wengi walikuwa wamerejea katika taratibu za kawaida za maisha. Zipo athari katika sekta mbalimbali hasa za kiuchumi kama vile sekta ya utalii na mauzo ya nje kwa mazao kama vile maua.

Katika nchi nyingi bado serikali zinachukua hatua ngumu ili kuweza kukabiliana na janga la korona. Kadiri muda unavyokwenda zimekuwepo juhudi mbalimbali katika ngazi za kitaifa na kimataifa kukabiliana na janga hili.

Katika maeneo tuliyokuwa tunapambana kukabiliana na athari za korona hususan katika nyanja ya elimu, hadi mwezi Juni mwishoni watoto wengi walikuwa wamerejea mashuleni.

Hivyo namna yetu ya utekelezaji wa majukumu kulingana na shughuri zetu pia ulibadilika.

Kabla ya kusonga mbele na kuendelea na kazi zetu tathmini ya utendaji wakati wa korona ilifanyika. Pamoja na idadi ya watoto tuliokuwa tumewafikia lakini pia wafaidika wa zoezi tulilolifanya walisema kwamba zoezi zima lilikuwa limewasaidia kurejea masomo ya darasani na hivyo kuwaweka katika utayari wa kuendelea na masomo kwa urahisi zaidi. Baadhi walipendekeza zoezi liwe la kudumu. Utendaji wetu ulitokana na uhitaji katika dharura iliyojitokeza kutokana na korona.



Mwezi wa Septemba washiriki katika zoezi la uwezeshaji katika kipindi cha korona walipongezwa kwa ushiriki wao katika zoezi hilo. Kila mmoja alituzwa cheti kuonesha kutambua kujitoa kwao katika kipindi chote hicho.

## MAADHIMISHO YA TAREHE 17 OKTOBA MWAKA 2020

Maadhimisho ya tarehe 17 Oktoba mwaka huu yalifanyika katika ukumbi wa shule ya sekondari ya Turiani iliyopo Magomeni. Kamati ya maandalizi ilikuwa imeanza kazi ya maandalizi ya maadhimisho haya tangu mwezi wa Agost. Mwaka huu kutokana na janga la korona maandalizi yalichelewa tofauti na miaka mingine.

Kamati ya maandalizi ilikutana kupanga na hatimaye mada ya siku ilipotolewa, ilituwezesha kutoa mwelekeo wa maandalizi ya siku yenyewe. Kamati kutokana na ushirikiano mkubwa na mshikamano uliokuwepo iliweza kuratibu na kuandaa mwelekeo wa siku yenyewe.Tarehe 17 mwaka 2020 tofauti na mwaka uliopita, ilikuwa siku angavu iliyokuwa imashehenezwa na jua lililokuwa linang'arisha nuru njema. Wadau kutoka maeneo yetu ya shughuri wakiwa maridadi walijumuika kuja kuadhimisha siku hii ya Oktoba 17.

Pamoja na wadau, nao marafiki kutoka maeneo mbalimbali walifika kujumuika pamoja nasi.. Mwezi Oktoba 17 mwaka huu, tukio hili lilikuwa linafanyika kipindi cha kampeni za uchaguzi nchini Tanzania. Tarehe 17Oktoba ilikuwa siku kumi tu kabla ya siku yenyewe ya uchaguzi. Kamati ilikuwa inatarajia kukusanya jumla ya washiriki mia mbili lakini wengi kati ya viongozi wa serikali katika ngazi ya kata hawakuweza kuhudhuria kwa ajili ya kampeni, lakini pia hata wale waliofanikiwa kuhudhuria hawakuweza kukaa kwa muda mrefu. Hivyo pamoja na wanaharakati, marafiki na wafanyakazi wa serikali katika ngazi mbali mbali jumla ya watu walioshiriki ilikuwa kama mia moja na zaidi kidogo hivi.

miongoni mwao tulikuwa tumekaribisha pia viongozi na wafanyakazi katika ngazi mbalimbali katika serikali za mitaa.Mada kuu ya mwaka huu ilikuwa ***"Kuchukua hatua kwa pamoja ili kufikia haki za kijamii na mazingira kwa wote".*** Kamati ya maandalizi katika kutafakari na kufahamu kauli mbiu hii ilitambua umuhimu wa kushirikisha wadau kuijadili ili waifahamu na kuangalia umuhimu wake katika maisha ya kila siku. Suala kubwa lilikuwa namna ya kuhakikisha ujumbe unawafikia wadau wote. Hivyo kamati iliandaa maswali matatu ambayo iliamuliwa yajadiliwe wakati wa maadhimisho na matokeo yake yajumuishwe pamoja. Hii itawasaidia washirikia kufikiri na kubuni ushiriki katika kuboresha mazingira yao lakini pia kutambua haki zao katika jamii.

Maswali yaliyokuwa yameandaliwa yalikuwa:

1. **Tunaelewa nini juu ya haki za jamii na mazingira?**
2. **Hatua zipi tunaweza kuchukua ili kuboresha haki za jamii na mazingira katika maeneo yetu?**
3. **Je ni athari zipi zinazoikumba jamii katika kuzifahamu haki za jamii na mazingira yao**

Majumuisho ya majibu ya maswali haya yametolewa katika taarifa ya

*(Muhtasari wa mjadala uliofanyika siku ya tarehe, 17 Oktoba 2020 katika ukumbi wa shule ya Sekondari Turiani Dar es salaam).*

Awali maadhimisho ya siku hii baada ya kufunguliwa kwa sala kutoka katika dini za Kikristo na Kiislamu ikafuatiwa na kutambulishwa siku na ufafanuzi wa mkusanyiko, maana ya siku pia kuelezea yote yanayohusiana na siku hii. Ulisomwa ujumbe kutoka kwa mkurugenzi wa shirika la kimataifa na kisha zilisomwa shuhuda. Shuhuda mbili za kwanza zilionesha namna watu wanavyoonewa, kudhulumiwa na kutumiwa bila kulipwa fidia. Kwamba wanahitajika pale tu wanapokuwa na faida baada ya hapo hawafai tena. Lakini pia ukweli kwamba juhudi zao katika kupambana na maisha ya kila siku zinaandamwa na lawama na uonevu. Shuhuda ya mwisho ilijikita zaidi katika haki za jamii, maisha ambayo pia yanaweza kutokana na dhuluma inayotokana pengine na nguvu ya pesa.

Shuhuda hii ya tatu itatayarishwa peke yake kwa sababu haikuwa imetayarishwa kwa ajili ya kutolewa siku ya Oktoba 17. Ilikuwa na mguso na wengi walijisikia kutokwa machozi. Shuhuda hii itaandaliwa na kuhifadhiwa katika kumbukumbu zetu. Washiriki siku hii walikuja kushiriki siyo kushuhudia tukio. Tulicheza muziki na mirindimo ya ngoma kutoka katika kikundi cha ngoma kilichokuwa kinatumbuiza. Pamoja na ushiriki huu wa furaha lakini pia tulikumbushana kuhusu wenzetu waliokuwa wanakabiliana na madhila ya janga la korona. Tulishiriki , tulifurahi na kujifunza kwa pamoja.Washiriki walifurahia namna siku ilivyokuwa imeandaliwa. Walishiriki katika maadhimisho, hawakuja kushuhudia.

Washiriki walielewa mada ya mwaka huu na kwa pamoja walitafakari namna ya kuiishi. Hii ilidhihirishwa na taarifa kwamba hata pale walipokuwa wanarejea nyumbani waliendelea kuijadili mada na matukio ya siku.

***Matokeo.***

Kwa ujumla watu waliifurahia sana siku hii.

Washiriki walifanikiwa kuelimishana kwa njia ya mjadala na hivyo kuielewa vema zaidi mada ya siku, walicheza muziki na ngoma na kufurahi kwa pamoja.

Michango yao na malalamiko kuhusiana na masuala ya elimu ilichukuliwa na afisa elimu aliyekuwepo kwa ajili ya ufuatiliaji.

**<u>Ukaribisho wa wanatimu Micol, kuagana na Salma na Saleh</u>**

Mwezi wa Novemba mwaka 2020 timu ya Tanzania ilipokea wafanyakazi wawili wa kujitolea. Hawa ni Micol na Damien ambao ni mke na mume na watoto wao wawili. Hawa wametoka makao makuu Mery, Ufaransa.

Salma na Saleh walikuwa katika timu ya Dar es salaam. Wanakwenda kujiunga na Reuben ambaye ni rafiki wa muda mrefu wa ATD. Yeye amekuwa anatembea katika falsafa za mwasisi wa ATD Joseph Wresinski. Salma na Saleh wanakwenda kumwongezea nguvu katika shughuri anazozifanya.







Shuhuda mbalimbali zilitolewa mbele ya hadhara ilifika katika maadhimisho ya siku ya kuutokomeza umaskini





TAFAKARI NA MAJADILIANO PIA YALICHUKUA NAFASI, SHUKRANI KWA WOTE WALIOSHIRI-






Wasanii na vijana wa ATD walitumbuiza kwa ngoma za asili na dansi. Shukrani kwa kikundi cha JITAMBUE na vijana wa ATD dunia ya nne Tanzania.

**Wasiliana nasi**

ATD Dunia ya nne - SLP 61786 - Dar es salaam.

Simu namba - +255 754 501 628

Barua pepe - national.team.tanzania@atd-fourthworld.org

Tovuti ya Kiswahili: www.atd-fourthworld.org/where-we-are/africa/tanzania